

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

Simu Na: +255 (026) 2963405
Nukushi: +255 (026) 2963406

Barua Pepe : ps@utumishi.go.tz
Tovuti : <http://www.utumishi.go.tz>



Jengo la Taaluma Na.1,
Chuo cha Masomo ya Biashara
na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MB) APONGEZWA NA KAMATI YA
KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA
KUSIMAMIA UTENDAJI MZURI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI
YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA
BORA**

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa wamempongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angellah J. Kairuki (Mb) kwa kusimamia vema utendaji wa taasisi za umma zilizopo chini ya ofisi yake.

Pongezi hizo zimetolewa na wajumbe wa kamati hiyo mara baada ya Mhe. Kairuki kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kwa kamati hiyo.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Mhe. George M. Lubeleje (Mb), alisema miongoni mwa eneo ambalo Mhe. Kairuki anastahili pongezi ni la ukaguzi na usimamizi mzuri wa zoezi la uhakiki wa kaya masikini zilionufaika na fedha za Mpango wa Kususuru Kaya Masikini nchini (TASAF) na kubaini kaya 63,813 zilionufaika na mpango huo, huku zikiwa hazina sifa.

Pia, Mhe. Lubereje alimpongeza Mhe. Kairuki kwa usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ambapo kupitia mpango huo, Serikali imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima 1,068 na

viongozi 219 wa vyama vya wakulima kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kukuza mitaji katika Halmashauri za Wilaya za Mwanga, Meru, Mbinga, Sumbawanga, Kalambo, Korogwe, Karagwe na Kilombero.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Mwanne I. Mchemba (Mb) alimpongeza Mhe. Kairuki kwa usimamizi mzuri wa Taasisi zote zilizopo chini ya Ofisi yake na kumtaka kuendelea na jitihada hizo.

“Nakupongeza kwa usimamizi mzuri wa Chuo cha Utumishi wa Umma tawi la Tanga ambacho kinafanya vizuri sana, hivyo ni jukumu la ofisi yako kuendelea kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamirifu”, alisema Mhe. Mchemba.

Kwa upande wake, Mhe. Kairuki aliihidi kamati hiyo kuendelea kutekeleza majukumu yake kikamirifu katika kuzisimamia Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi yake ili ziweze kutoa huduma bora kwa umma.

Akizungumzia changamoto ya uwepo wa kaya zilizonufaika kimakosa na fedha za Mpango wa kunusuru Kaya Masikini nchini, Mhe. Kairuki aliihidi kamati hiyo kuwa atahakikisha Maafisa wote wa Serikali waliohusika wanakuchukuliwa hatua za kisheria.

IMETOLEWA NA:
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI,
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA
UTAWALA BORA,
DODOMA.
29 Machi, 2017**